# SHIRIKA LA MELI ZANZIBAR

## SHIRIKA LA MELI LINATANGAZA NAFASI KWA MSAMBAZAJI WA VYAKULA KWA MIKAHAWA MINNE YA MELI YA MV MAPINDUZI II

*Wasiliana nasi uwe sehemu ya timu inayohudumia abiria wetu kwa vyakula na vinywaji vyenye ubora wa hali ya juu katika safari za baharini.*



**MV Mapinduzi II**

**Taarifa Kuu:**
Shirika la Meli Zanzibar linatangaza nafasi ya kibiashara kwa wasambazaji wa vyakula na vinywaji kwa ajili ya huduma katika mikahawa minne (4) iliyomo kwenye meli ya kisasa ya MV Mapinduzi II.

**Sifa za Muombaji:**

1. **Uzoefu na Uelewa wa Mazingira:**
    - Upendeleo utawekwa kwa wale walio na uzoefu wa kusambazia kwenye meli, hoteli kubwa, au mikahawa ya kimataifa.
    - Uelewa wa taratibu za usafirishaji bandarini na vigezo vya usalama.
    - Watumishi wa Kampuni watatakiwa kuvaa sare muda wote wa safari na ‘reflectors’ wakati wa kuingia na kutoka bandarini.
2. **Leseni na Vibali Kamili: (Usajili)**

- Kuwa na leseni halali ya biashara na vibali vyote vinavyohitajika kufanya kazi ndani ya bandari.
- Muombaji anatakiwa aambatanishe vyeti vya Mlipa kodi.
- Watumishi wa Kampuni hawatalala ndani ya Meli. Watumishi watakuwa wanakuja kuhudumia abiria mwanzo wa safari na kushuka Meli ikifika sehemu husika.
- Watumishi wa Kampuni watahitajika kukata vitambulisho vya kuingia bandarini.
- Kuwasilisha vielelezo vya uzoefu wa kazi zinazofanana ikiwa ni pamoja na mikataba ya uzoefu kwa kazi inayoombwa.
- Muombaji anatakiwa kuambatanisha nakla ya Cheti cha ZFDA.

3. **Kiwango cha kutoa 'Offer'**
    - Muombaji ainishe kwa barua kiwango cha fedha atakachoweza kutoa kwa Shirika kwa kila mwezi 'offer'.

**Aina za Bidhaa Zinazohitajika:**

- **Vyakula Vilivyo Bora:** Nyama (ng'ombe, kuku, kondoo), Samaki, mboga mboga matunda, viazi, nafaka n.k.
- **Vinywaji:** Kahawa, chai, vinywaji baridi, maji ya kunywa na juisi.
- **Vifaa vya Jikoni:** Vifaa vidogo vidogo vya jikoni, vyombo vya kupikia, vyombo vya meza (sahani, bilauri, vijiko, uma), na vifaa vya usafi.
- **Bidhaa Zingine:** Vifaa vya kufungia, vifaa vya usalama wa chakula, na bidhaa nyinginezo zinazohitajika kwenye jiko la Meli.

**Jinsi ya Kuomba:**

- Muombaji anatakiwa awasilishe maombi yake kwa barua kwa kumuandikia Mkurugenzi Muendeshaji Shirika la Meli Zanzibar.
- Muombaji awasilishe maombi hayo yakiwa kwenye bahasha iliyofungwa vizuri kwa kuainisha aina ya kazi anayoiomba.

Anuani ya Barua:

**Mkurugenzi Muendeshaji,**

**Shirika la Meli Zanzibar,**

**S.LP. 80.**

**Zanzibar.**

Maombi hayo yawasilishwe si zaidi ya Ijumaa tarehe 17/02/2026 saa za kazi.

**Mawasiliano:**
Ikiwa una sifa, tafadhali tuma barua pepe yako kamili kwa:

**Barua Pepe:** [info@shipco.go.tz]
**Kichwa cha barua: USAMBAZAJI WA VYAKULA- MV MAPINDUZI II**
**Muhusika:** [ Idara ya Masoko, Utafiti na Mipango]

---

***Shirika la Meli Zanzibar***
*"Tunajivunia kuhudumia wateja wetu kwa usalama."*